

★ MONGELLA: MWANZA ITAKUWA TOFAUTI

★ DC AZINDUA BWENI LA KISASA MISUNGWI

Hutolewa: Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mwanza

# Mwanza Kwanza



/Mwanzakwanza

Toleo Februari, 2021

Uzalishaji

Miundombinu

Kutoka Wilayani

“KATIKA KUTOA TUNAPOKEA”

## Sasa ni

# JP Magufuli Bridge

Daraja la JPM au JP Magufuli ndilo jina jipya kwa daraja hili ambalo ujenzi wake bado unaendelea ukitazamiwa kukamilika mwaka 2024, yaani miaka mitatu kuanzia sasa. Limepewa jina la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt John Pombe Magufuli. Dkt Magufuli amewapa wananchi daraja ili kupunguza shida zao, ametoa akapokea jina. **UKURASA 3**



**Jafo:**  
**Mwanza**  
**mko**  
**vizuri**  
UK 4

Wananchi Ukerewe wajenga shule nne **UK 8**

Ilemela wanufaika na Shilingi bil. 1.1 **UK 10**





Ujumbe wa

# Mkuu wa Mkoa

John Mongella

## Mwanza itakuwa tofauti

**K**aribuni tena wasomaji wa Mwanza Kwanza katika toleo la kwanza la jarida letu la mtandani kwa mwaka huu mpya 2021. Ninawataka wote mwaka mpya wenye kheri na baraka tele, tukiendelea na majukumu yetu ya kujenga uchumi wa nchi kila mmoja kwa nafasi aliyokuwa nayo.

Ni wajibu wetu kama watu binafsi, taasisi au serikali kujiweka malengo kwa vipindi tofauti tofauti. Unapoanza mwaka mpya ni muda mzuri pia kutafakari yote yaliyotokea katika mwaka unaoisha na kuanzalia kwa mwaka mpya kitu gani kipya cha kufanya na kwa namna gani tunaboresha yale ambayo tumeshindwa kuyatimiza kwa ufasaha kwa mwaka ulioisha.

Kama mkoa kuna mengi yamefanyika na yanaendelea kufanyika ikiwa ni sehemu ya mkakati wa serikali ama katika ngazi ya kitaifa au katika ngazi ya mkoa. Katika ngazi ya kitaifa tumeona utekelezaji wa miradi ya kimkakati ambayo imeanza

mwaka jana na inaendelea. Kama mkoa ni majukumu ya kutimiza katika kuhakikisha miradi hii inatekelezwa vizuri na inakamilika katika muda uliopangwa. Kama mkoa, wale wanaofanyakazi katika miradi hii wanapaswa kufanyakazi kwa juhudi na maarifa, uaminifu na kujitotoa; wale wanaosambaza vifaa na zana za ujenzi wanatokiwa kufanya hivyo vizuri wakitoa huduma bora inayotakiwa na wale wanaopaswa kusimamia basi wafanye hivyo kwa umakini mkubwa.

Katika ngazi ya mkoa, kuna shughuli nyingi zinaendelea kama ujenzi na utoaji huduma katika hospitali, uboreshaji wa barabara zetu na uimarishaji wa elimu kwa kujenga madarasa na kusimamia ufundishaji ili vijana wetu wanaomaliza elimu ya msingi na sekondari wapate ufaulu mzuri na kuendelea na masomo ya elimu ya juu. Tuna majukumu pia ya kuhakikisha kwamba mkoa wetu u salama na hili ni jukumu la kila mmoja wetu.

Tangu kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu na kuapishwa kwa Baraza jipya la Mawaziri mwaka jana, tumeshuhudia ziara za viongozi mbalimbali katika mkoa wetu, akiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt John Pombe Magufuli ambaye alikwenda kukagua ujenzi wa Daraja la JP Magufuli. Daraja hili lime-tembelewa pia na Waziri Mkuu Mheshimiwa Kasimu Majaliwa Majaliwa, Makama wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Seif Sharif Hamad na viongozi wengine mbalimbali. Huu ni ujumbe muhimu kwetu sote kwamba tunakazi kubwa mbele yetu, tuji- toa kwa kiasi kikubwa.

Miradi ya Kimkakati ya Kitaifa na ile ya mkoa imetembelewa na mawaziri wengi ambao wanataka kuona jinsi kazi zinavyondolea katika eneo hili huku wakitoa ushauri na maelekezo mbalimbali ambayo tunapaswa kuyafanyia kazi kadri inavyopaswa.

Ziara hizi za viongozi wetu zinamaanika kubwa sana kwetu;

kwamba serikali inajitahidi kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi kama ambavyo mgombea wake wa Urais na sasa Rais Mheshimiwa Dkt Magufuli na wabunge ambao wengine wameteuliwa kuwa mawaziri walivyokuwa wakii- nadi wakati wa kampeni za uchaguzi mwaka jana. Kama wananchi tuliahidiwa hivyo, tukakubali na kuwachagua, basi jukumu letu kubwa ni kushirikiana nao katika kutekeleza majukumu yaliyo mbele yetu kama wafanyakazi wa serikali na binafsi, wafanyakazi wa taasisi za umma na binafsi na wengine wote.

Hadisani wazikwambatunajitahidi kutekeleza na hii inanipa Imani kubwa sana kwamba Mwanza itakuwa na sura tofauti ndani ya miaka mitano ijayo. Serikali ishaweke fedha nyingi sana, ni sisi tu kufanya kazi.

Nawataka wote usomaji mwe- ma wa jaridi hili.

*John V. Mongella*  
**Mkuu wa Mkoa Mwanza**



Gazeti hili linatolewa:  
Ofisi ya Mkuu wa  
Mkoa wa Mwanza



**+255 028 2501037**



**ras.mwanza@tamisemi.go.tz**



**www.mwanza.go.tz**

Regional Drive  
Mkabala na Ofisi za  
TRA P.O. Box 119,  
Mwanza

**Katibu Tawala:**  
**Kitengo Cha Habari:**

**Wahariri washauri:**

Emmanuel Tutuba  
Abel Ngapemba  
Remija Salvatory  
Mha. Aron Kalondwa  
Patrick Karangwa  
Fabian Gapchojiga  
Thabita Masota  
Dkt. Silas Wambura  
Abdul Mzee  
Innocent Keya  
Barnabas Mkwayu



**+255 28 2501037**  
**+255 0784 273 588**  
**+255 0783 317 118**

**Usanifu / Matangazo:**

**+255 0657 929 650**



**“KATIKA KUTOA TUNAPOKEA”**

# Sasa ni JP Magufuli Bridge

**NA ABEL NGAPEMBA**

**W**akati Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara (TANROAD) Mhandisi Patrick Mfugale anatoa jina rasmi la daraja kubwa linalojengwa mkoani Mwanza, jambo moja likaja katika kichwa changu...kwanini jina linabadilishwa wakati lile lilokuwapo lingekuwa zuri tu kuwa jina rasmi kwani lilikuwa linaakisi muungano wa wilaya mbili ambazo zinatenganihwa na kipande cha Ziwa Victoria, Kigongo kwa wilaya ya Misungwi na Busisi kwa wilaya ya Sengerema; Daraja la Kigongo- Busisi.

Lakini baadaye nikakumbuka usemi mmoja ambao unasema, “Katika Kutoa ndiyo tunapokea”. Maneno haya yalitolewa na Mtakatifu Francisco wa Assis ambayo yapo katika moja ya sala maarufu kwa Wakristo, hasa wakatoliki. Sala hiyo imepewa jina la “Bwana unifanye kuwa chombo cha amani yako”.

Ni sala ambayo Mtakatifu Francisco wa Assis anamuomba Mungu awe mtu wa msaada kwa binadamu wengine. Anaomba pale palipo na chuki aeneze upendo, palipo na mashaka apeleke imani, pasipo na matumaini apeleke matumaini, palipo na giza apeleke mwanga na pale penye huzuni apeleke furaha. Anaendelea kumwomba Mungu amjalie asitafute kufarjiwa bali yeye ndiye mfarji, asitafute kupendwa bali yeye ndiye apende akisema kwamba kwamba kwa kuwa “Katika Kutoa ndipo Tunapokea”.

Daraja la JPM au JP Magufuli ndi-

lo jina jipya kwa daraja hili ambalo ujenzi wake bado unaendelea ukitazamiwa kukamilika mwaka 2024, yaani miaka mitatu kuanzia sasa. Limepewa jina la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt John Pombe Magufuli. Dkt Magufuli amewapa wananchi daraja ili kupunguza shida zao, ametoa akapokea jina.

Daraja hilo litakalokuwa na urefu wa kilomita 3.2 litagharimu jumla ya shilingi bilioni 699.2 na tofauti na miradi mingine ya ujenzi, hili litajengwa kwa fedha za ndani ambazo zinatokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ya serikali ikiwemo kodi.

Suala kwamba ujenzi wa daraja utatokana na fedha za ndani lilitolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt John Magufuli Desemba 2019 wakati anaweka jiwe la msingi la ujenzi huo.

Kuna mengi alisema wakati anaweka hilo jiwe la msingi likiwemo ukombozi wa wananchi wa maeneo hayo, “ujenzi wa daraja hili utakuwa mkombozi kwa wananchi wa maeneo haya” alisema na kuongeza kwamba Wakazi wa Kanda ya Ziwa na nchi za Maziwa Makuu watanufaika pia.

Alisema uamuzi wa kujenga daraja hilo unatokana na changamoto mbalimbali za usafiri kupitia katika kivuko hicho, changamoto ambazo alikuwa anazijua kwa sababu alikuwa Waziri wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa takribani miaka 17.

Changamoto nyingi ambazo wananchi walikuwa wakizipata kwa nyakati tofauti hususan wakati vivuko vinapopata hitilafu ama kwa

kuharibika au wakati wa kufanyiwa matengenezo ya kawaida ya kiufundi.

Siku chache baada ya Mhandisi Mfugale kutembelea daraja hilo na kusema kwamba litaitwa Daraja la JPM (JP Magufuli Bridge), Dkt Magufuli mwenyewe alitembelea kuangalia maendeleo ya ujenzi wake.

“Daraja hili mimi ninahistoria nalo”, alisema Dkt Magufuli na kuelezea stori ya yeye kwenda kuchumbia Sengerema akitokea Mwanza na kukwama wakati wa kurudi baada ya kivuko kuharibika akiwa na pikipiki.

“Nilienda hadi kwenye mwalo ambako kulikuwa na mtumbwi unavusha watu, moyo ukakataa. Mtu na familia yake waliingia katika mtumbwi na mabaiskeli. Mimi nikaondoka nikazunguka Kamanga na nilipofika Mwanza nikapata habari kwamba mtumbwi ule ulizama na kuua watu 11”, alisema.

Anasema wakati anagombea akiona iwe moja ya ahadi zake wakati wa kampeni ili kufanya ujenzi aokoe maisha ya watu, “Mara ya kwanza watu hawakuamini, waliona haiwezekani wakaona naota na wengine wakisema ni maneno tu ya kampeni”.

Baada ya hii stori ya Rais Magufuli, hata ile kuhaji kwangu kuhusu jina ikapoteza nguvu, nikaona kwa nini kulikuwa na haja ya kutoa jina lile kwa mtu ambaye katika siku zote, tangu akiwa Waziri wa Ujenzi alikuwa akipigania urahisi wa usafiri kwa wananchi wa maeneo hayo. Lakini ndipo ilipokuja kichwani pia sala ya Mtakatifu Francisco wa Assis kwam-

ba “Katika kutoa ndipo Tunapokea”.

Jina la Daraja la JPM limepokelewa na wananchi wa Mwanza na mikoa ya jirani kama ambavyo Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. John Mongella alivyosema wakati Mhandishi Mfugale anatangaza kuwekwa kwa jina rasmi la daraja hilo kwamba inaonekana waliopendekeza jina kama walikuwa katika mawazo wa wananchi.

“Daraja katika kivuko hiki limetajwa mara nyingi sana katika awamu zote tano lakini ufadhili ulionekana ni shida kupatikana. Daraja hili ni la kiuchumi. Ni njia fupi zaidi kati ya Congo ya Mashariki na Kenya”, alisema Mongella.

Dkt. Magufuli pamoja na ujenzi kuwa umeshaanza tangu Februari mwaka jana na wajenzi wakisema utakamilika ndani ya muda, bado amewasisitiza wahusika kuhakikisha kwamba daraja hilo linakamilika kabla ya muda wake uliopangwa.

“Nina matumaini watamaliza kabla ya muda. Ninawaomba contractors, consultant na wasimamizi Tanroad, pesa ipo, pesa hakuna tatizo, pesa ya watanzania ipo. Wafanye kazi usiku na mchana, wawe na shift”, anasema.

Mwanza Kwanza ilitembelea daraja hilo na kuona mafundi wakielelelea na ujenzi wa daraja la muda ambalo limefikia urefu wa mita 600 ukienda sambamba na ujenzi wa daraja lenyewe kwa kuchimba mashimo ambayao nguzo za daraja hilo zitasimikwa.

Wakati ujenzi huo unaendelea, huduma za usafiri wa feri za MV Mwanza na MV Misungwi ulikuwa ukiendelea ambako abiria, malori na

mizigo ya aina mbalimbali ilikuwa ikivushwa kwa kupishana.

Daraja hilo linajengwa na mkandarasi kutoka China, China Civil Engineering Group Limited kwa kushirikiana na kampuni nyingine ya Railway 15 na umejumuisha wataalam mbalimbali wa Kitanzania ambao wanashirikiana kukamilisha ujenzi wake. Mradi huo unatarajiwa kutoa jumla ya ajira 1600 kwa wakazi wa Mkoa wa Mwanza.

Ujenzi wa daraja hili kwa fedha za ndani unadhahirisha uwezo wa Tanzania katika kutekeza miradi mikubwa yenye manufaa makubwa kwa uchumi wa nchi na wananchi wake. Jambo ili llinatosha kuwapa imani watanzania wote kwamba kodi wanazolipa hazipotei bali zinatumiwa kwa manufaa yao wenyewe kwa wananchi wake.

Rais Magufuli wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi huo aliwataka wafanyabiashara na watanzania kwa ujumla kuendelea kulipa kodi na kusisitiza kuwa ulipaji wa kodi unaimariasha uhuru watanzania kufanya nchi iheshimike kimataifa na duniani kutokana na kuwa na uwezo wa kusimamia shughuli zake kubwa za uchumi.

Kukamilika kwa ujenzi wa daraja hili ambalo litawanufahisha pia nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kutaharakisha shughuli za usafirishaji wa mizigo na abiria katika ushoroba wa Ziwa Victoria sanjari na kuunga mkono juhudi za Serikali za kuipeleka nchi kwenye uchumi wa kati wa viwanda.





# Mwanza mko vizuri - Jafo

NA MWANDISHI WETU

Tangu kuapishwa kwa mawaziri wapya katika kipindi cha pili cha Awamu ya Tano ya Uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt John Pombe Magufuli, viongozi mbalimbali wamekuwa wakimiminika mkoani Mwanza kuangalia shughuli mbalimbali za kiuchumi ambazo zinatekelezwa katika mkoa huu. Viongozi wa Kitai-fa, mawaziri na viongozi wa taasisi mbalimbali wametembelea miradi mbalimbali ya maendeleo na kutoa maelekezo kadhaa.

Mmojayaviongoziambaowalitembelea miradi ambayo inatekelezwa mkoani Mwanza ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mheshimiwa Selemu Jafo ambaye ndiye haswa mwenye dhamana na mkoa na halmashauri zake kama ilivyo kwa mikoa mingine nchini. Alifanya ziara ya siku mbili kutembelea Jiji la Mwanza, Manispaa ya Ilemela, Halmashauri ya Kwimba, Halmashauri ya Sengerema na Halmashauri ya Buchosa. Katika maeneo hayo, alitembelea kukagua miradi ambayo inatekelezwa na idara ambazo zinasimamiwa na TAMISEMI.

Miradi ambayo Jafo alikwenda kuikagua ni Ujenzi wa Dampo unao-fanywa na Jiji la Mwanza, Ujenzi wa hospitali ya wilaya ya Kwimba, Ujenzi wa Stendi ya mabasi na maegesho ya malori ya Nyamhongolo katika wilaya ya Ilemela na ujenzi wa Jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza ambao unachangiwa kwa pamoja na Jiji la Mwanza na Manispaa ya Ilemela. Miradi mingine ambayo alikagua ni Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Sengerema na ujenzi wa ofisi za Mkurugenzi wa Halmashauri ya Buchosa.

Kimsingi ni ziara ambayo inewatia moyo watendaji na wananchi katika maeneo hayo kutokana na sifa ambazo Jafo amezitoa kwa miradi ambayo ameikagua katika ziara yake hiyo ya mkoa. Ni eneo moja ambalo Waziri Jafo hakulidhishwa na usimamizi wake ambako ni Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema ambako alikuta kuna tatizo katika uwepo wa hati ya eneo ambalo hospitali imejengwa, ubora wa jengo la hospitali ya wilaya na pia kuwepo kwa taarifa zinazokanganya kuhusu ukubwa halisi wa eneo hilo la hospitali.

Mkanganyiko huo ukamlazimisha Jafo kutembelea pia na eneo ambalo linatarajiwa kujengwa Kituo Kikuu cha mabasi cha Sengerema ambako nako alikutana na tatizo la ulipaji fidia.

Jafo alianza ziara yake kwa kufungua mafunzo ya siku mbili wa walimu wanaofundisha watoto wenye mahitaji maalum ambao ulilenga kutoa mafunzo kwa walimu hao ili wakawafundishe wenzao namna ya kuwabaini watoto wenye mahitaji maalum nchi nzima ili wote waandikishwe shule.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa katika mafunzo hayo, lengo la serikali ni kuhakikisha ndani ya wiki mbili watoto wote wenye mahitaji maalum kati ya umri wa miaka minne hadi sita wawe wamebainishwa na kufanyiwa taratibu za kuandikishwa shule.

Akifungua mafunzo hayo, Jafo alisema kwamba kundi hili kwa muda mrefu limekosa fursa, lakini ni kundi lenye manufaa sana kwa taifa na kama wangeendelea kutochukua hatua taifa litapoteza vijana wengi, "Bila kufanya hivi tutapoteza vijana wengi na itakuwa dhulma kubwa sana kwa watoto hawa".

Baada ya kufungua mafunzo hayo, Waziri alitembelea eneo lilipojengwa Dampo na kuridhishwa na ujenzi

**Tunaendelea kukushukuru, ziara zako za mara kwa mara hazijatua-cha bure kwani umekuwa dira yetu. Uliyoyaelekeza tutayasimamia kwa dhati nasi tutakosoana kwa dhati na kusifiana kwa dhati na tunaweka nguvu ili miradi yote iishe kwa wakati"**

John Mongella, Mkuu wa Mkoa



wake, hasa baada ya kuambiwa kuwa watendaji walitembelea madampo mengine ili kujifunza kwa lengo la kuepuka kurudia makosa ambayo wenzao watakuwa wameyafanya wakati wa utekelezaji.

"Endeleeni kutembelea kwa wengine mkajifunze. Nendeni Tanga, dampo la Tanga ni the best. Tunataka miradi hii ikae muda mrefu na mitambo ambayo inatumika hapa itumike kwa muda mrefu, zaidi ya miaka 15. Hakikisheni kunakuwa na matumizi sahihi ya mitambo," Alisema Jafo.

Katika halmashauri wa Misungwi, Jafo alikwenda kukagua ujenzi unaondelea wa Hospitali ya Wilaya ya Kwimba ambao gharimu yake ni kiasi cha shilingi bilioni 2.07 ambako kunatakiwa kuwapo jengo ya Utawala, Wodi ya Wazazi, Jengo la Mionzi, jengo la wagonjwa wa nje, Maabara, jengo la kufulia, mashimo

ya majitaka na mfumo wa Tehama. Hadi sasa, majengo ya Maabara na wagonjwa wa nje yamekamiliwa kwa asilimia 98.

"Wakati nakuja hapa mara ya kwanza, hali ilikuwa ya kuhuzunisha sana, na hata hizi fedha mlizopewa hazikuwa katika bajeti yenu bali ni huruma tu ya Rais Magufuli kwa wananchi wake. Majengo yamesimamiwa vizuri sana. Nilichokiona hapa sicho nilichokiona wilaya ya Chemba, hili jengo ni zuri na ninashawikisha kwenda kumwambia Mheshimiwa Rais aongeze fedha", alitoa ahadi Jafo kwa watendaji wa Halmashauri hiyo.

Ujenzi wa hospitali hiyo ambayo itarajiwa kuhudumia wananchi 462,855 ulianza Juni mwaka jana kwa ujenzi wa majengo mawili ya awali ambayo ni ya maabara na ya wagonjwa wa nje baada ya serikali kutoa Shilingi milioni 500 za ujenzi.

Mradi mwingine ambao Jafo alikuwa ni wa Ujenzi wa Stendi ya mabasi na maegesho ya malori ya Nyamhongolo uliopo katika Manispaa ya Ilemela ambao gharimu yake ni Shilingi bilioni 28. Mradi huo unasehemu mbili ambazo ni Ujenzi wa Stendi ya mabasi na Ujenzi wa Maegesho ya malori.

Sehemu ya Ujenzi wa stendi ya mabasi unajumuishi miundombinu ambayo ni maegesho ya mabasi, jengo la abiria litakalokuwa na maduka, migahawa, sehemu za tiketi, benki na sehemu ya kusubiria mabasi. Miundombinu mingine ni Jengo la biashara ambalo litakuwa na maegesho ya magari madogo na vibanda vya maduka vya rejareja. Utekelezaji wake umefikia asilimia 60

Sehemu ya maegesho ya malori unaambatana na miundombinu ya nyumba ya kulala wageni (hosteli) yenye vyumba 100, eneo la maegesho malori 100 kwa wakati mmoja, vyoo vya kulipia, godaumi lenye uwezo wa kutunza mizigo ya mita za ujazo 5,400 na karakana ya magari. Utekelezaji wa sehemu hii ya mradi umefikia asilimia 65.

Utekelezaji wa mradi huu mkubwa ulianza Julai mwaka jana na unatarajiwa kukamilika Mei mwaka huu.

Baada ya kukagua mradi huo, Jafo alisema kwamba ujenzi huo ni kitu muhimu sana ambacho amekiona, "Nimefarijika sana na ujenzi huu. Stendi hii ni kubwa na ni mfano katika Kanda ya Ziwa na ni mfano kwa Tanzania kwa ujumla", alisema.

Aliwataka viongozi wa Ilemela kuanza kuangalia namna gani wataendesha stendi hiyo kubwa ili kuhakikisha kwamba fedha iliyowekezwa hapo inarudi na kuhakikisha kwamba kama inapewa kampuni kusimamia, basi iangalie isije ikajikuta Manispaa yenyewe haina kauli tena mbele ya mwendesha huyu.

Katika siku ya kwanza ya ziara yake, Waziri alitembelea Uwanja wa Ndege wa Mwanza kukagua ujenzi wa Jengo la abiria ambalo Septemba mwaka 2019 ambao unatarajiwa kumalizika Aprili mwaka huu. Fedha za ujenzi wa jengo hili zinatoka Jiji la Mwanza ambao wanatoa Shilingi bilioni 2.2, Manispaa ya Ilemela Shilingi bilioni 1.8 na serikali kuu ambako zinatoka Shilingi bilioni 11.6. Ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 80.

Siku ya pili ya ziara yake, Waziri alitembelea Wilaya ya Sengerema na kukagua ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Sengerema na eneo lililotengwa kwa ajili ya Stendi Kuu ya Mabasi na kisha kuelekea Buchosa ambako alikagua jengo la Mkurugenzi wa Halmashauri ya Bushosa pamoja na Ujenzi wa Hospitali ambao tayari umekamilika na sasa wanasubiri vifaa.

Katika ziara hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mheshimiwa John Mongella alimshukuru waziri na kueleza kwamba mafanikio ambayo ameyaona yanatokana na maelekezo ya waziri na viongozi wengine wa serikali ambao wamekuwa wakitoa dira na maelezo mbalimbali.

"Tunaendelea kukushukuru, ziara zako za mara kwa mara hazijatua-cha bure kwani umekuwa dira yetu. Uliyoyaelekeza tutayasimamia kwa dhati nasi tutakosoana kwa dhati na kusifiana kwa dhati na tunaweka nguvu ili miradi yote iishe kwa wakati", alisema Mongella.



# Watoto wote wataingia darasani: Mongella

NA REMIJA SALVATORY

**M**kuu wa Mkoa wa Mwanza, Mheshimiwa John Mongella amesema kwamba wanafunzi wote waliochaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari wataanza masomo kama ilivyopangwa mwaka huu kwa kuwa ujenzi na ukarabati wa madarasa utakamilika kwa muda uliopangwa.

Mongella alitoa kauli hiyo baada ya kukagua ujenzi wa madarasa na shule mpya kwa ajili ya wanafunzi ambao wanatakiwa kuanza kidatu cha kwanza mwaka huu kama alivyoelekeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kasimu Majaliwa Majaliwa kwamba mikoa yote wahakikishe watoto wote waliofaulu darasa la saba kuingia kidato cha kwanza.

Mongella alikagua ujenzi na ukarabati wa madarasa katika Jiji la Mwanza ikiwa ni sehemu ya ziara zake za kutembea wilaya za mkoa kukagua utekezaji wa maagizo ya serikali kuhusu kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa ili kuhakikisha watoto wote waliomalizia na kufaulu darasa la saba wanaingia darasani.

“Nimethibitisha kwamba watoto wote waliomaliza darasa la saba na kufaulu wataingia shule katika Jiji la mwanza. Kazi mnayofanya ni kubwa sana, ila msibweteke hasa ikizingatiwa Jiji ndio kuna watoto wengi zaidi katika mkoa huu, pamoja na Halmashauri ya Ilemela,” alisema Mongella.

Katika ziara hiyo, Mongella alitembelea shule za sekondari za Pamba iliyopo katika kata ya Pamba, Mahina iliyopo katika Kata ya Mahina, Mhandu katika kata ya Mhandu, Shamaliwa katika kata ya Igoma na Igoma iliyopo katika kata ya Kishiri.

Shule nyingine ni Lwanhima na Sahwa zilizopo katika kata ya Lwanhima, Buhongwa na Bulale zilizopo Kata ya Buhongwa, Mkolani katika kata ya Mkolani, Nyabulogoya katika Kata ya Nyegezi na Luchebele katika Kata ya Luchebele.

Awali akitoa taarifa ya utekezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Mkurugenzi wa Jiji la Mwanza, Bw. Kiomoni Kibamba alisema kwamba walikuwa na upungufu wa madarasa 120 kutokana na ongezeko la watoto 6,018 waliofaulu mwaka jana.

“Jiji la Mwanza linataraji kusajili wanafunzi 11,418. Idadi hii inaleta upungufu wa madarasa 120 kutokana na ongezeko la wanafunzi 6,018



## 1,325

**Pamoja na ujenzi na ukarabati huo, Jiji pia limeshatengeneza madawati 1,325 yenye thamani ya Shilingi milioni 106**

waliofaulu ukilinganisha na miundombinu iliyopo...halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa kushirikiana na jamii imeanza ujenzi wa ukarabati wa jumla ya madarasa 67 ambapo madarasa 57 yenye thamani ya Shi-

lingi 564,902,135 na madarasa 10 yenye thamani ya Shilingi 43,148,300 yanakarabatiwa,” alisema Kibamba.

Katika hayo madarasa 57, Shule ya Sekondari Pamba yanajengwa madarasa sita, Buhongwa madarasa matano, Lwanhima madarasa 11, Igoma madarasa 10, Mkolani madarasa saba, Mahina madarasa matano, Luchebele madarasa matano, Shamaliwa madarasa matano, Bugarika darasa moja, Mapango madarasa matano, Mbugani madarasa mawili na Nyabulogoya madarasa matatu.

“Sambamba na ujenzi huu na ukarabati, Halmashauri ya Jiji la Mwanza kwa kushirikiana na wananchi imeanza ujenzi wa shule mpya mbili katika Mtaa wa Sahwa Kata ya Lwanhima pamoja na Mtaa

wa Bulale katika Kata ya Buhongwa. Jumla ya madarasa 10 yanaendelea na ujenzi katika shule hizo,” alisema Bw. Kibamba katika taarifa yake.

Ujenzi na ukarabati wa shule hizo unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Januari tayari kwa watoto kuingia kidato cha kwanza mwanzoni mwa Februari.

Pamoja na ujenzi na ukarabati huo, Jiji pia limeshatengeneza madawati 1,325 yenye thamani ya Shilingi milioni 106 kwa shule za Lwanhima, Mirongo, Mahina, Nyegezi kila moja ikipata madawati 250 na Mhandu ambayo imepata madawati 325. Shilingi milioni 70 zimetengwa kuendelea kutengeneza madawati kwa shule nyingine na pia kufanya ukarabati wa madawati ambayo yameharibika.



## HUDUMA ZA AFYA MWANZA



# Hili ni eneo la kimkakati kuwekeza: Tutuba

NA ABEL NGAPEMBA

“Tunazipongeza jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano ya Mhe. John Joseph Magufuli zilizofanyika katika kupunguza vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi wa watoto wachanga, na tunatoa shukrani za dhati kwa Ofisi ya Mkuu wa mkoa na Mganga Mkuu wa mkoa kwa ushirikiano mkubwa tunaondolea kuupata katika utekelezaji wa shughuli za afya katika Mkoa wa Mwanza.”

Ni kauli ya Bw. Sulaiman Shahabuddin, Afisa Mtendaji Mkuu wa Huduma za Afya wa Aga Khan Health Services, Africa Mashariki alipokuwa akimkabidhi Katibu Tawala wa mkoa wa Mwanza Bw. Emmanuel Tutuba mashine nane za kutolea dawa za usingizi, vifaa tiba na samani vyote kwa ujumla vikiwa na thamani ya Sh. Bil. 1.5.

Akipokea vifaa hivyo, Bw. Tutuba amesema kwamba Aga Khan Health Services wamefanya uamuzi sahihi kabisa kutoa msaada katika Jiji la Mwanza kwa sababu Mwanza ni eneo la kimkakati katika kufanya ubia na serikali.

“Ukiwekeza Mwanza unahudumia watu zaidi ya milioni 3.8, lakini kwa jiografia yetu unahudumia watu wengi zaidi kutoka mikoa mingine

nane ya Kanda ya Ziwa. Lakini pia ni wazi unahudumia nchi nyingine jirani zinazotuzunguka kwa sababu wote wanakuja kufuata huduma Mwanza”, alisema Bw. Tutuba.

Ameishukuru Aga Khan Health Services kwa msaada wa vifaa tiba na samani uliotolewa na pia kwa kazi ya ujenzi wa majengo ishirini na saba ya huduma za afya jijini Mwanza ambao umekuwa ukifanyika kwa vipindi tofauti.

Mashine nane za kutolea dawa za usingizi ni kwa ajili ya hospitali za wilaya ya Nyamagana, Misungwi, Ukerewe, Kwimba na Magu na pia katika Kituo ya Afya cha Buzuruga kilichopo Ilemela, Kituo cha Afya cha Kakobe kilichopo Buchosa na Kituo cha Afya cha Sengerema kilichopo halmashauri ya Sengerema.

Vitu vingine vilivyotolewa ni pamoja na taa 12 za vyumba vya upasuaji, vitanda 12 vya upasuaji, mashine nane za kuangalia mwenendo vya wagonjwa, oxygen concentrators nane, suction mashine 12, phototherapy, neonatal incubators and C- section kits, majokofu manne ya kuhifadhi damu, water bath 10, vitanda vya wagonjwa na magodoro 336, ngazi 17 za chumba cha kujifungulia, meza 62, viti 185 na mabenchi 58.



Msaada huo ni sehemu ya kazi za Mradi wa Uboreshaji wa upatikana-ji wa huduma za Afya kwa wazazi na watoto ujulikanao kama IMPACT (Improving Access to Reproductive

Maternal and Newborn Health). Mradi wa IMPACT unatekelezwa na mashirika ya Aga Khan Development Network ambayo ni Aga Khan Health Services Tanzania, Aga Khan

Foundation Tanzania na Aga Khan University kwa ufadhili wa Serikali ya Watu wa Canada (Global Affairs Canada). Lengo la mradi ni kushirikiana na serikali katika jitihada za kupunguza vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga. “Mradi huu unafanya kazi katika vituo vya kutolea huduma za afya 80 ndani ya halmashauri zote nane za Mkoa wa Mwanza”, alisema Meneja wa mradi, Edna Selestine.

Hadi sasa kupitia mradi huu, IMPACT kwa kushirikiana na serikali ya Mkoa wa Mwanza imejenga majengo 27 ya kutolea huduma za mama na mtoto ikiwa ni pamoja na majengo nane yenye vyumba vya kufanyia upasuaji. Ndani ya majengo hayo pia yamewekwa vifaa tiba muhimu kwa ajili ya kusaidia utoaji huduma za msingi kwa wakina mama na watoto.

**Ukiwekeza Mwanza unahudumia watu zaidi ya milioni 3.8, lakini kwa jiografia yetu unahudumia watu wengi zaidi kutoka mikoa mingine nane ya Kanda ya Ziwa.**

Emmanuel Tutuba

# Mitano ijayo tukijivunia mitano iliyopita

Wodi ya wanaume ya Hospitali ya wilaya ya Nyamagna iliyojengwa kwa mapato ya ndani



moja ya vikundi vya vijana kijulikanacho kwa jina la SOMA BAGS kilichopo Luchelele ambacho kimenufaika na mkopo wa Jiji utolewao bila riba.

## Bil.30

Jiji limetumia zaidi ya Shilingi bilioni 30 katika miradi ya mbali mbali ya maendeleo katika sekta ya Afya, Elimu, Mazingira pamoja na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kwa muda wa miaka mitano (2015- 2020)

lingi bil 1.4 katika hospitali ya wilaya ya Nyamagna, Ujenzi wa zahanati tano za kisasa za Isamilo, Mkuyuni, Bulale, Mhandu na Isebanda pamoja na upanuzi wa kituo cha afya cha Igoma, zaidi ya bilioni 1.2 zimetumika kukamilisha ujenzi na uboreshaji wa huduma katika miradi hii.

Kwenye Elimu, Jiji la Mwanza limejenga madarasa 214 katika shule za Msingi na sekondari, matundu 614 ya vyoo katika shule za Msingi na sekondari, na kutengeneza madawati 16,354 kwa ajili ya shule za msingi na sekondari.

Kwa upande wa mazingira, katika kuhakikisha jamii inakuwa salama na uchafuzi wa mazingira, Jiji limejenga Dampo la Kisasa kwa gharama ya Shilingi bil. 8.9 ambao ni mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Jitihada hizi za Jiji hazikuishia katika miundombinu tu katika jiji, bali pia limefanya uwekezaji mkubwa kwa wananchi wake katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Uwekezaji huu ni katika kuviwezesha vikundi vya vijana, wakinamaa na walemavu ambapo vikundi 669 vilipata mikopo isiyo na riba yenye jumla ya thamani ya Shilingi bil. 2.4.

Katika kipindi hiki cha miaka mitano, mengi yaliyofanyika, tena kwa kutumia fedha zitokanazo na mapato ya ndani ni cha kujivunia kwani yote yalifanyika kwa kufuata nyayo za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Jiji la Mwanza litaendelea kuisi katika falsafa ya "Hapa Kazi Tu" ili kuwahudumia wananchi katika kuwaletea maendeleo.



**Kushoto: Kiwanda cha kufyatua matofali kilichopo Buhongwa ambacho kinachomilikiwa na Jiji la Mwanza Jiji4:**

**NA MARTIN SAWEMA, AFISA HABARI JIJI**

**N**i jambo linalojulikana kwa kila mtanzania kuwa serikali ya Awamu ya Tano imetekeleza kwa kishindo mambo yaliyokuwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2015 – 2020 hususani katika sek-

ta ya miundombinu, afya, elimu, maji na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

Katika kuiangazia Halmashauri ya Jiji la Mwanza kuishi dhana ya "Hapa Kazi Tu" katika kuwahudumia wananchi na kutatua kero za wananchi. Halmashauri ya Jiji la Mwanza imetekeleza kwa kishindo miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta ya Afya, Elimu,

Mazingira pamoja na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

Utekelezaji wa miradi katika sekta zote hizo Jiji la Mwanza kwa muda wa miaka mitano (2015- 2020), Jiji limetumia zaidi ya Shilingi bilioni 30 katika miradi ya maendeleo.

Katika sekta ya Afya, Jiji limejenga wodi ya wanaume kwa gharama ya shi-

# Wananchi Ukerewe wajenga shule nne

NA STEVEN MSENGI,  
AFISA HABARI UKEREWE

**N**aibu Katibu Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Bw. Gerald Mweli ameupongeza uongozi wa Wilaya ya Ukerewe na wananchi wa kata za Bukungu, Kagunguli, Nkilizya na Ilangala kwa kujenga shule mpya katika maeneo yao na hivyo kuwapunguzia adha wanafunzi kutembea umbali mrefu na kuvuka maji kuhudhuria masomo.

Bw. Mweli alitoa pongezi hizo baada ya kutembelea Shule mpya ya Sekondari ya Ilangala na kukagua ujenzi ambako hadi sasa madarasa sita yameshajengwa na manne kati yake yameshakamilika yote yakiwa na thamani ya Shilingi milioni 46.4 Ujenzi huo unaenda sambamba na ujenzi wa matundu 18 ya vyoo.

Fedha za ujenzi wa sekondari hiyo inatokana na michango ya wananchi wakishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe. Kwa kutambua michango ya wananchi katika



ujenzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Bi. Ester Chaula ameahidi kwamba halmashauri itatoa bati bandari tatu na saruji mifuko 100 kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya walimu.

Baada ya ukaguzi huo wa shule,

Bw. Mweli amewataka wakaguzi wa elimu kukamilisha haraka ukaguzi wa shule hizo ili zipate usajili tayari kwa kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza ifikapo Februari mwaka huu.

Shule ya Sekondari ya Ilangala ina-

**Tumetoa Shilingi milioni 120 zinazotokana na kodi ya mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji madarasa ili kuwezesha kupokea wanafunzi wa darasa la kwanza na kidato cha kwanza mwaka huu**

Bi. Ester Chaula

tarajiwa kuhudumia shule za msingi saba na jumla ya visiwa 12 vya Ilangala. Shule zingine mpya za sekondari ambazo nazo zimejengwa na wananchi na zipo katika hatua ya mwisho kukamilishwa kama sekondari ya Ilangala ni Sekondari ya Bukungu, Buzegwe na Nkilizya.

Wakati huo huo Mkurugenzi Mtendaji wa Ukerewe Bi. Ester Chaula amesema kwamba wametoa Shilingi milioni 120 zinazotokana na kodi ya mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji madarasa ili kuwezesha kupokea wanafunzi wa darasa la kwanza na kidato cha kwanza mwaka huu.

Kauli ya Bi. Chaula imekuja baada ya kumkabidhi Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Mhe. Cornel Magembe, mifuko 1,190 ya sar-

uji na bati bandari tatu vyote vikiwa na thamani ya Shilingi million 25.9.

Katika makabidhiano hayo, Mhe. Magembe alisema kwamba vifaa hivyo vya ujenzi vilivyotolewa ni muhimu katika kukamilisha madarasa kuelekea kufunguliwa kwa shule.

“Waziri Mkuu Alitoa mwisho wa ukamilishaji wa miundombinu ya madarasa kabla ya tarehe 28 mwezi wa pili mwaka huu, lakini Ukerewe tumejitokea kukamilisha mwisho wa mwezi huu,” alisema Magembe.

Magembe amewataka watendaji wa kata wanaokabidhiwa saruji hizo kuwashukuru wananchi na serikali za vijiji kwa kuen-delea kushirikiana na Halmashauri katika kuunga mkono juhudi za kuboresha elimu.





# MISUNGWI



TOLEO LA FEBRUARI, 2021



## DC azindua bweni la kisasa Misungwi

NA THOMAS LUTEGO

**M**kuu wa Wilaya ya Misungwi, Mhe. Juma Sweda amezindua bweni la kisasa wasichana la katika katika Shule ya Sekondari Misungwi ambalo ujenzi wake umegharibu Shilingi milioni 120.

Akizungumza katika uzinduzi wa bweni hilo, Sweda aliupongeza uongozi wa Sekondari hiyo kupitia kwa Mkuu wa Shule hiyo ambaye amekuwa mstari wa mbele na ameonyesha kwamba ni mchapakazi na mwenye moyo wa kupenda maendeleo ya jamii.

“Hili ni bweni ambalo kimsingi ni bweni la mfano unaweza ukaangalia hata Mkoa wa Mwanza bweni kama hili unaweza usilipate na bweni ambalo lina huduma zote na ni bweni la kisasa sana” Alisisitiza Sweda.

Ameeleza kwamba bweni hilo litaleta na kuongeza chachu ya kusoma kwa wanafunzi na kuwataka wanapomaliza wasisahau Wilaya ya Misungwi na kuendelea kuikumbuka daima katika maisha yao. Aliwataka wanafunzi hao kusoma kwa bidi na kuongeza ufaulu kwani wametatuliwa kero yao.

“Serikali itaendelea kuboresha

**Serikali itaendelea kuboresha miundombinu na mazingira ili msome vizuri na kuongeza ufaulu zaidi. Nawaomba mlitumie bweni hili vizuri kwani lina mahitaji yote yanayopaswa kuwepo bwenini kwani ni la kisasa zaidi”**

Mhe. Juma Sweda

miundombinu na mazingira ili msome vizuri na kuongeza ufaulu zaidi. Nawaomba mlitumie bweni hili vizuri kwani lina mahitaji yote yanayopaswa kuwepo bwenini kwani ni la kisasa zaidi”, alisema.

Naye Mkuu wa shule hiyo, Bw. Ananius Mbandwa ameeleza katika taarifa ya mafanikio ya shule hiyo kwamba shule hiyo imeanzishwa mwaka 1994 na kufanikiwa kuanza kidato cha tano mwaka 2016 katika mchepuo wa EGM na CBG

Katika matumizi ya fedha ya ujenzi huo, Sh. Mil 40 zimetokana na mapato ya ndani ya shule n ash.

Mil 60 zimetoka serikali kuu.

Bweni hilo lina uwezo wa kuchukua vitanda 40 vya aina ya deka. Jumla ya wanafunzi 80 wanakaa katika bweni hilo, wanafunzi 50 wa kidato cha sita na 30 wa kidato cha tano.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hal-mashauri ya Wilaya ya Misungwi, Bw. Kisena Mabuba amewapongeza viongozi wa shule hiyo kwa ushirikiano na juhudi za kuleta mabadiliko ya elimu wanazoendelea kuzifanya hususani katika matokeo ya wa wanafunzi wa kidato cha nne na sita.



# Ilemela wanufaika na Shilingi bil. 1.1



**NA VIOLA MBAKILE,  
AFISA HABARI ILEMELA**

**K**ila mamlaka za Serikali za mitaa Tanzania zinao wajibu wa kutenga asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Hii ni kwa mujibu wa kanuni ya 4. -(1) ya kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imeendelea kutekeleza agizo hilo la kutenga asilimia 10 kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani na kutoa mikopo hiyo kwa wanawake, vijana na walemavu. Katika mgawo huo, asilimia nne huelekezwa kwa wanawake, asilimia nne nyingine kwa vijana na asilimia mbili inayobaki hupewa watu wenye ulemavu.

Ili kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatunika kwa malengo yaliyokusudiwa, wataalamu kutoka Idara ya Maendeleo ya Jamii ya Manispaa ya Ilemela kwa kushirikiana na madiwani wa viti maalum, huhakikisha wanawajengea uwezo kwanza kwa kuwapa elimu na mafunzo mbalimbali juu ya matumizi sahihi ya fedha hizo.

Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imekuwa ikitoa mikopo hiyo tangu ilipoanzishwa mwaka 2012, ikitoa kwa makundi ya wanawake na vijana kupitia kamati ndogo za mikopo zilizoundwa katika ngazi ya kata na kuratibiwa na maafisa maendeleo ya Jamii kata na kupitishwa na kamati za Maendeleo za kata (WDC) na kisha kupitishwa katika vikao vya kamati za kudumu za Halmashauri.

Awali fedha hizo za mkopo kwa

makundi hayo mawili zilikuwa zikitolewa kwa masharti ya riba ya asilimia 10 kwa mwaka. Mwaka 2017 serikali iliziagiza mamlaka za serikali za mitaa kuongeza kundi la walemavu katika upatikanaji wa mikopo hiyo.

Ili kuweza kuwasaidia Wanawake, vijana na walemavu kujikwamua kiuchumi, mwaka 2018 serikali iliamua kuwa mikopo hiyo itolewe bila riba ili kuwapa fursa wanawake, vijana na walemavu kwa ajili ya kuanzisha miradi kwa wingi ya kujikwamua kiuchumi kwani suala la riba limekuwa kikwazo kwa makundi mengi kuweza kukopa na kurejesha mikopo kwa wakati.

Vikundi vingi vinavyopatiwa mikopo hiyo hujishughulisha na biashara ndogondogo, utengenezaji wa batiki, sabuni za maji, kilimo cha bustani, biashara ya dagaa na samaki na ufugaji wa kuku.

Kikundi cha Masaligula kilichopo Kata ya Sangabuye ni mojawapo ya vikundi vinavyofaidika na mkopo huu wa Halmashauri na hujishughulisha na mradi wa uuzaji wa dagaa pamoja uendeshaji wa mgahawa.

Mhasibu wa kikundi hicho Bi. Elizabeth Bahati anasema kuwa hii ni mara ya pili kwa kikundi chao kupata mkopo huu ambapo awamu ya kwanza walipata fedha kiasi cha Shilingi milioni mbili na awamu ya pili wamepata mkopo wa Shilingi milioni tatu.

Aidha anaongeza kuwa, mkopo huu umewasaidia kukuza biashara yao kwani hapo awali walikuwa wakilangua dagaa na kutembeza kwenye mabeseni lakini kwa sasa wanaweza kununua dagaa kwenye magunia toka kwa wavuvi na kuwauzia wanaotembeza kwenye mabeseni. Aliongeza kuwa mafanikio mengine yaliyopatikana kutokana na mkopo

huu, ni kuwa wameweza kuwasomesha watoto kupitia fedha wanazopata kupitia biashara hiyo.

Amewashauri wakinamama kujiunga na vikundi mbalimbali ili waweze kupata mkopo huo kwani hauna riba na ni wenye masharti nafuu huku akiwaasa wale ambao wamekuwa hawarejeshi mkopo kuhakikisha wanarejesha kwa wakati ili kujenga uaminifu. Pamoja na hayo kwa niaba ya wanufaika wa mkopo huo, Bibi Elizabeth ameishukuru serikali kwa kuanzisha utaratibu huo wa utoaji wa mkopo usiokuwa na riba

kwani umewarahisishia maisha na kuwaletea maendeleo.

Pamoja na mafanikio hayo zipo changamoto mbalimbali ambazo Halmashauri imekuwa ikikabiliana nazo katika suala hili la utoaji wa mikopo ambazo ni pamoja na baadhi ya vikundi kutokurejesha mkopo kwa wakati, vikundi vingi vya vijana vinavyopata mkopo huu husambaratika hivyo kupelekea kutokurejesha mkopo. Kwa upande wa vikundi vya walemavu wamekuwa wakidhani mkopo huu ni ruzuku hivyo hawarejeshi kabisa.

Ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imejiwekea mikakati mbali ya kuhakikisha kuwa fedha hizi zinaendelea kuwanufaisha makundi haya na kuweza kujikwamua kiuchumi baadhi ya mikakati hiyo ikiwemo ni ufuatiliaji wa marejesho ambapo ipo timu maalum ya ufuatiliaji inayohusisha wataalam wa maendeleo pamoja na madiwani wa viti maalum ikiwa ni pamoja na kuendelea kuwapa elimu ya urejeshaji wa mikopo.

Kwa kipindi cha miaka mitano ili-yopita, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imefanikiwa kutoa mikopo ya fedha kiasi cha Shilingi bilioni 1.194 isiyoyana na riba kwa makundi ya wanawake vikundi 364, vijana vikundi 95 na walemavu vikundi 15. Kwa mwaka 2015/2016 zilitolewa kiasi cha Shilingi mil 22; mwaka 2016/2017 Shilingi mil 252; mwaka 2017/2018 Shilingi bil. 116 na mwaka 2018/2019 Shilingi mil. 501

Katika mwaka wa fedha unaoendelea wa 2019/2020 hadi sasa Ilemela imefanikiwa kutoa kiasi cha Shilingi mil. 303 kwa vikundi 76 vya wanawake (mil.248), vikundi 15 vya vijana (mil. 40) na vikundi sita ya walemavu (mil. 15).

Ipo mikakati mbalimbali ambayo imewekwa katika kuhakikisha kuwa makundi haya yanawezeshwa na kujikwamua na suala zima la umasikini ikiwemo kuhakikisha kuwa makundi haya yanapewa mkopo mkubwa katika kila kata ambao utawawezesha kutekeleza mradi mkubwa ambao utakuwa wa mfano kwa jamii, pia kuendelea kutoa mikopo midogo midogo kwa makundi hayo.

Kwa mwaka huu wa fedha, Halmashauri ya Ilemela inakadiriya kutumia jumla ya Shilingi mil. 857.3.



# SENGEREMA

Mwanza Kwanza



TOLEO LA FEBRUARI, 2021



## RC aipongeza Halmashauri Sengerema

NA SYLVANUS MDALAMI,  
AFISA HABARI SENGEREMA

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. John Mongella ameupongeza uongozi na Halmashauri ya wilaya ya Sengerema kwa kusimamia miradi mbali mbali ya maendeleo.

Mongella aliyasema hayo alipokuwa ziarani katika Halmashauri ya Sengerema na kutembelea Zahanati ya Kasenyi ambako

kulikuwa na mradi wa ujenzi wa wodi ya wazazi ambao ulipangwa kutekelezwa na uongozi wa zahanati hiyo. Katika ujenzi huo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt John Pombe Magufuli alichangia shilingi milioni 10 kwa ajili ya kuiboresha.

Uongozi uliamuakuanzishaujenzi wa wodi ya wazazi kwa kutenga fedha kupitia vyanzo vyake vya ndani ili kuwasaidia akina mama ambao walikuwa wanapata shida wakati wa kujifungua katika zaha-

Vijana changamkieni fursa ya kuwa na watoto wa kutosha kwani Serikali imeamua kuboresha huduma kwa jamii hivyo hakuna mtoto anayeweza kupata shida na ndiyo maana serikali imeamua kutoa Elimu bure kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne

RC John Mongella

nati hiyo. Ujenzi umekamilia hivi sasa na wakinamama wameanza kutumia majengo hayo.

Kwa upande wake Mganga Mkuu

wa wilaya ya Sengerema Dkt. Peter Mahu amesema. "sisi kama wasimamizi wakuu wa masuala ya afya tumejipanga kuhakikisha wakina

mama wajaawazito wanapata huduma bora katika kipindi chote cha ujauzito hadi kujifungua ikiwa ni pamoja na kuhakikisha zahanati hii inakuwa na wataalamu wa kutosha".

Mhe. Mkuu wa mkoa amewataka vijana kuchangamkia fursa ya kuwa na watoto wa kutosha kwani Serikali imeamua kuboresha huduma kwa jamii hivyo hakuna mtoto anayeweza kupata shida na ndiyo maana serikali imeamua kutoa Elimu bure kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne.

